# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.08: Msimu wa Kilimo 2025/26* *Tathmini ya Disemba 11 -20, 2025 na Matazamio kwa Kipindi cha Disemba 21-31, 2025*



**MUHTASARI**

- Mvua zinazotarajiwa zitasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao.
- Wakulima wanashauriwa kufuatilia mazao kwa ukaribu huku wakishirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao.
- Wadau wote wa kilimo wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.



## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilisababisha sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kusogea kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, kati, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi, hali ambayo iliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo. Vile vile, uwepo wa upepo wenye unyevunyevu uvumao kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa Pwani, uliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, pwani ya kusini na nyanda za juu kusini magharibi. Pia, vipindi vya mvua katika maeneo machache ya pwani ya kaskazini, kusini mwa nchi na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2025

Katika kipindi cha dikadi, maeneo mengi nchini yalipata mvua kati ya milimita 11 hadi 150 kwa siku kumi. Hata hivyo, maeneo mengi ya mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro yalipata mvua kati ya milimita 1 na 100 kwa siku kumi kama inavyoonekana kwenye kielelezo.




Kielelezo 1: Jumla ya mvua kwa siku kumi kwa kipindi cha Disemba 11-20, 2025

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2025

Katika dikadi hii, baadhi ya maeneo nchini yalipata mvua ambayo ilisaidia kuongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji wa mazao. Hata hivyo hali ya upungufu wa mvua wa muda mrefu hususan katika mikoa ya Pwani na Tanga wilaya ya Muheza-Mlingano umeathiri ukuaji wa mazao. Pia upungufu wa mvua hususan kwa mikoa ya Singida, Dodoma, Mtwara umesababisha kuchelewesha upandaji wa mazao ya Msimu na wakulima katika maeneo hayo waliendelea na maandalizi ya mashamba.

Kwa maeneo yanayopata mvua za Vuli hususan kanda ya Ziwa Victoria na ukanda wa pwani ya Kaskazini, mahindi yapo katika hatua kutoa mbelewele. Katika mkoa wa Kagera mahindi yapo katika hatua ya kutoa kukomaa wakati katika mkoa wa Mwanza mahindi yapo katika hatua ya kubumba.

Kwa upande wa maeneo yanayopata mvua za Msimu, wakulima waliendelea na upandaji wa mazao na baadhi ya maeneo husussan mikoa ya Njombe, Rukwa na Songwe mahindi yapo kwenye hatua ya ukuaji. Hata hivyo katika mkoa wa Tabora mahindi yapo katika hatua ya kuota wakati mkoa wa Mbeya, wakulima waliendelea na shughuli za upandaji wa mahindi.

Kwa upande wa mazao ya muda mrefu, zao la korosho katika mkoa wa Mtwara lipo katika hatua ya kukomaa na wakulima waliendelea na uvunaji zao hilo, wakati zao la Kahawa likiwa katika hatua ya kutoa maua katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe.

Maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama vimepungua kwa baadhi ya maeneo kutoka na hali ya ukavu iliyokuwepo.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2025

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kilipungua husussan kwa maeneo ambayo yaliyokuwa na upungufu wa mvua kwa ujumla.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2025

Katika kipindi hiki migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa Dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kusogea kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, kati, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi, hali ambayo inatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Vile vile, uwepo wa upepo wenye unyevunyevu uvumao kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu unatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2025

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na abora), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mkoa wa Tanga, kaskazini mwa Morogoro na Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache hasa katika nusu ya mwisho ya dekadi.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), na nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), maeneo haya yanatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2025

Hali ya mvua inayotarajiwa nchini itasaidia kuongeza unyevu nyevu katika udongo. Vile vile, mvua hizi zitasaidia katika shughuli za upandaji wa mazao husussan kwa maeneo ambayo mvua za Msimu zimechelewa kuanza pia mvua hizi zitasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao mashambani.

**Ushauri:**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kufuatilia mazao kwa ukaribu huku wakishirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao huku wakichukua tahadhari kutokana na uwepo wa hali mbaya ya hewa ikiwemo mvua kubwa na vipindi vikavu vya muda mrefu vinapojitokeza.
  Aidha, wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa Mvua (nyanda za juu kusini magharibi, mikoa ya magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya kusini):** Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kumalizia shughuli za kupanda mazao husussan kwa wakulima ambao walikuwa hawajapanda bado.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kutunza mifugo katika maeneo mazuri na salama pamoja na kuangalia afya za mifugo mara kwa mara. Pia wanashauriwa kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali.

Ushauri huu umedhamiria kuongeza tija kwenye kilimo na kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya Hewa. Wadau wote wa kilimo wanahimizwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa ili kuwa na mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA DISEMBA 21-31, 2025

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka kidogo kutokana na mvua zinazotarajiwa. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)